# Kufanana na Kutofautiana kwa Konsonanti katika Msamiati wa Kipemba[1] na Kingazija[2]

*Sauda Uba Juma*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

**Ikisiri**

**Makala haya yanahusu ulinganishaji wa mfumo wa saui za konsonati baina ya Kipemba na Kingazija kwa lengo la kubaini mfanano na tofauti zilizopo baina yake. Data za makala haya zilikusanywa uwandani katika mazingira chasili ya wazawa wa lugha kupitia mbinu za hojaji na mahojiano. Matokeo tuliyoyapata kutoka kwa watoataarifa yameonesha kuwapo kwa mfanano na tofauti za mfumo wa sauti za konsonanti katika Kipemba na Kingazija. Hata hivyo, pamoja na tofauti za hapa na pale, tunathubutu kusema kuwa, Kipemba na Kingazija ni lugha ambazo zinatokana na lugha-mame moja, kwani tofauti hizo ndogondogo zilizojitokeza, imebainika kuwa zimetokana na utengano wake wa muda mrefu pamoja na umbali wa kijiografia uliopo miongoni mwake.**

**Maneno Muhimu**: konsonati, msamiati, sauti, lugha-mame.

## Utangulizi

Makala haya yanalenga kulinganisha mfumo wa sauti za Konsonanti za Kipemba na Kingazija na kuona jinsi zinavyofanana na kutofautiana. Azma ya ulinganinishi huo ni kuthibitisha au kukanusha kwamba Kipemba na Kingazija zinazotokana na lugha chanzi moja au ni lugha ambazo hazihusiani. Jambo lililotusukuma kufanya hivyo ni kutokana na misigano miwili kinzani iliyopo miongoni mwa wanazuoni kuhusu kadhia hii. Upande mmoja unadai kuwa Kingazija ni miongoni mwa lahaja za Kiswahili. Huu unawakilishwa na wanazuoni kama Chiraghdin na Mnyampala (1977), Kipacha (2003) na Massamba (2017). Upande wa pili una mtazamo kuwa Kingazija si miongoni mwa lahaja za Kiswahili bali ni lugha inayojitegemea. Huu

[1] Kinazungumzwa katika Kisiwa cha Pemba kilichoko takribani kilomita 50 Kaskazini Mashariki mwa Kisiwa cha Unguja katika bahari ya Hindi. Aidha, Kisiwa hiki kiko umbali wa kilomita 40 Mashariki mwa jiji la Tanga. (Juma, 2019).

[2] Kinazungumzwa katika Kisiwa cha Ngazija ambacho ni miongoni mwa fungu-visiwa vinne vinavyopatikana nchini Komoro. Viko katika Bahari ya Hindi baina ya Madagaska na Msumbiji pia, vimepakana na Pwani ya Afrika Mashariki na Pwani ya Msumbiji. Visiwa vya Komoro viKo umbali wa kilomita 300 kutoka Pwani ya Kaskazini ya Msumbiji na pia kutoka Kaskazini mwa Madagaska Kipacha, (2003).

unawakilishwa na Nurse na Spear (1985), Nurse (1989) na Nurse na Hinnebusch (1993) .

Misigano ya pande mbili hizi inatupa matokeo yanayosailika na pia inasababisha tatizo la ugumu wa kuelewa iwapo Kingazija ni miongoni mwa lahaja za Kiswahili au kinyume chake. Hivyo, makala haya yanalenga kulinganisha mfumo wa konsonanti za Kingazija na za lahaja mojawapo ya Kiswahili ambayo ni Kipemba ili kubaini namna zinavyofanana na zinavyotofautiana. Kipemba kimeteuliwa kutokana na tajiriba aliyonayo mtafiti kuhusu lahaja hii, jambo ambalo limerahisisha mchakato mzima wakati ukusanyaji wa data. Makala haya yamegawanywa katika sehemu kuu tano zifuatazo: utangulizi, kiunzi cha nadharia, mbinu, matokeo na hitimisho.

## Kiunzi cha Nadharia

Nadharia ya Isimu Historia-Linganishi imetumika katika uchambuzi wa data za makala haya iliyoasisiwa na William Jones (1786). Jones alihudhurisha nadharia hii katika mhadhara wake uliohusu lugha ya Kisanskriti ambapo alibaini kuwa Kiyunani, Kilatini na Kisanskriti zinaelekea kuwa na chimbuko moja. Misingi mikuu ya nadharia hii ni miwili. Mosi, ulinganishi wa kisinkronia ambao unalinganisha lugha mbili au zaidi kama zilivyo hivi sasa ili kuona jinsi zinavyofanana na kutofautiana. Pili, kuzichunguza lugha kidikronia ambapo lugha mbili au zaidi zinaweza kuchunguzwa maendeleo yake katika kipindi mahususi cha kihistoria. Aidha, katika nadharia hii kuna mbinu kuu ijulikanayo kama Mbinu Linganishi[3]. Mbinu hii ndiyo inayotumika katika kulinganisha vipengele vyote vya kiisimu vinavyolinganishwa katika lugha mbalimbali. Hivyo, katika makala haya Mbinu Linganishi imetusaidi kuzilinganisha konsonanti za Kpemba na Kingazija na kubaini namna zinavyofanana na kutofautiana.

## Mbinu za Utafiti

Data za makala haya zimekusanywa uwandani katika maeneo ya Pemba na Ngazija. Vijiji ambavyo vimehusishwa kwa upande wa Pemba ni Mwambe na Shamiani ambavyo vinadaiwa kuwa wazungumzaji wake hadi hii leo bado wanaendelea kukitumia Kipemba halisi kuliko Kiswahili Sanifu (Juma, 2019). Kwa upande wa Ngazija eneo lililohusika ni Moroni kwa sababu ndilo eneo ambalo linafikika kwa urahisi kutokana na kuwa eneo hilo lina miundombinu mizuri ya barabara. Eneo la Bangwakuni limeteuliwa kwa kuwa lina wazungumzaji wengi wa asili ambao pia wanazungumza Kiswahili Sanifu jambo ambalo lilimrahishia mtafiti wakati wa ukusanyaji data. Itsinkudi ya Washili limeteuliwa kwa sababu ni eneo ambalo

[3] Mbinu ambayo inatumika sana katika Nadharia ya Isimu Historia-Linganishi ili kulinganisha lugha mbili au zaidi kwa lengo la kubaini iwapo lugha hizo zina mnasaba mmoja au la (Massamba, 2007, 2017).

inaaminika kuwa halina mwingiliano mkubwa na jamii nyingine; hivyo, wazungumzaji wake hawajaathiriwa sana na jamii zinazowazunguka.

Katika makala haya tulitumia mbinu ya hojaji yenye orodha ya maneno 200 ambayo ni msamiati wa msingi uliojumuisha kategoria mbalimbali za maneno. Msamiati huo uliandaliwa kutoka maktabani kwa kuzingatia mapendekezo ya (Swadesh, 1952) ya jinsi ya kuandaa msamiati wa msingi ambao ulihusu majina ya sehemu za mwili, maumbile ya asili, vitenzi vya asili, majina ya namba n.k. Kwa ujumla, mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata msamiati wa msingi uliochambuliwa ambao ulitumika kulinganisha konsonanti mbalimbali za Kipemba na Kingazija zilizotokea katika maumbo ya maneno hayo. Mbinu hii ilitumika kwa wale tu wanaojua kusoma na kuandika Kiswahili Sanifu. Watoataarifa waliojaza hojaji ni walimu 5 na wanafunzi 5 kutoka Pemba na mwalimu 1[4] na wanafunzi 9 kutoka Ngazija na kufanya jumla ya watoataarifa 20.

Mbinu ya mahojiano ilitumika kwa minajili ya kupata taarifa mbalimbali za kiisimu ambazo zilimsaidia mtafiti kupata data za mfumo wa sauti za konsonanti. Majadiliano yalihusisha watu ambao tayari wameonesha uelewa na mapenzi ya kuwa sehemu ya watoataarifa kupitia ushiriki wao katika mbinu ya hojaji. Mbinu hii ilitusaidia kuthibitisha msamiati wa msingi ulikaokusanywa kwa njia hii kabla ya uchambuzi. Katika kuitumia mbinu hii tulijadiliana na wazee kuhusu masuala mbalimbali yakiwemo ya kihistoria ya wazungumzaji wa Kipemba na Kingazija pamoja na vikundi vya walimu na wanafunzi kutoka katika maeneo husika. Lengo lilikuwa kuchunguza jinsi sauti zinavyotumiwa katika utamkaji wao wa maneno. Aidha, kupitia vikundi hivyo tulijadili msamiati wa msingi ili kuhakiki ukubalifu wa data zilizokusanywa. Katika kuzitumia mbinu hizo wakati mwingine maneno ya Kifaransa[5]yalitumika pale ilipoonekana kuwapo kwa ulazima wa kuyatumia katika Kingazija. Hivyo, tulilazimika kuwa na mkalimani aliyeweza kufasiri lugha ya Kiswahili, Kingazija na Kifaransa hasa kwa wale ambao hawakuifahamu vizuri lugha ya Kiswahili. Aidha, mtafiti alilazimika kutumia kinasasauti kurekodi mazungumzo mbalimbali yaliyojadiliwa katika vikundi vilikavyohusika.

## Matokeo

Wanaisimu na wataalamu mbalimbali wameziainisha sauti za lugha kwa kuzigawa katika makundi anuwai. Wataalamu wa awali kama vile (Jakobson na Halle, 1951) walijaribu kuzigawa sauti hizo katika makundi matatu ambayo ni irabu, viyeyusho na konsonanti. Baadaye (Chomsky na Halle, 1968) walizianisha sauti za lugha na kuzigawa katika makundi mawili makuu ambayo ni irabu na konsonanti. Kigezo cha mfumo wa sauti za Kipemba na Kingazija katika makala haya kimehusisha

[4] Mwalimu pekee anayefundisha Kiswahili Ngazija nzima.

[5] Maneno ya Kifaransa yalitumika kuondoa mkanganyiko pale ambapo neno la Kiswahili sanifu halikueleweka katika Kingazija.

kuziainisha na kuzilinganisha sauti mbalimbali za konsonanti ambazo zimebainika katika Kipemba na Kingazija na kubaini jinsi zinavyofanana na kutofautiana .

**Konsonanti**

Sauti za konsonanti hutamkwa kwa kuzuia mkondohewa kutoka mapafuni, ukipitia katika chemba ya kinywa, chemba ya pua na kutoka nje. Wakati wa utokaji wa sauti hizo, huathiriwa kwa kuzuiwa kwa kiasi kikubwa au kidogo kwa mkondohewa huo (Chomsky na Halle, 1968; Massamba, 2011). Tuangalie Jedwali Na. 1 ambalo linaorodhesha konsonanti za Kipemba na Kingazija:

**Jedwali Na. 1: Idadi ya Konsonanti za Kipemba na Kingazija**

| Na. | Otografia | Matamshi | Kipemba | Kingazija |
|---|---|---|---|---|
| 1. | b | [b] | b | b |
| 2. | pv | [β] | - | β |
| 3. | ch | [č] | č | č |
| 4. | $č^h$ | [$č^h$] | $č^h$ | - |
| 5. | d | [d] | d | d |
| 6. | f | [f] | f | f |
| 7. | g | [g] | g | g |
| 8. | th | [θ] | - | θ |
| 9. | dh | [ð] | - | ð |
| 10. | gh | [ɣ] | - | ɣ |
| 11. | h | [h] | h | h |
| 12. | j | [j] | j | j |
| 13. | dj | [ʤ] | - | ʤ |
| 14. | k | [k] | k | k |
| 15. | ky | [ky] | ky | - |
| 16. | $k^h$ | [$k^h$] | $k^h$ | - |
| 17. | l | [l] | l | l |
| 18. | ly | [ly] | ly | - |
| 19. | m | [m] | m | m |
| 20. | n | [n] | n | n |
| 21. | ny | [ɲ] | ɲ | ɲ |
| 22. | ng' | [ŋ] | ŋ | ŋ |
| 23. | p | [p] | p | p |
| 24. | $p^h$ | [$p^h$] | $p^h$ | - |
| 25. | r | [r] | r | r |
| 26. | tr | [ʈ] | - | ʈ |
| 27. | dr | [ɖ] | - | ɖ |
| 28. | s | [s] | s | s |
| 29. | sh | [š] | š | š |

| **Na.** | **Otografia** | **Matamshi** | **Kipemba** | **Kingazija** |
|---|---|---|---|---|
| 30. | t | [t] | t | t |
| 31. | t$^{h}$ | [t$^{h}$] | t$^{h}$ | - |
| 32. | ts | [ts] | - | ts |
| 33. | dz | [dz] | - | dz |
| 34. | v | [v] | v | v |
| 35. | w | [w] | w | w |
| 36. | y | [y] | y | y |
| 37. | z | [z] | z | z |
| **Jumla** | | **37** | **28** | **30** |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Katika Jedwali Na. 1 imebainika kuwa lina jumla ya konsonanti 37 zilizojitokeza katika Kipemba na Kingazija kwa idadi tofauti. Aidha, uchunguzi uliofanywa umebaini kuwa Kingazija kina idadi kubwa ya konsonanti 31 kikilinganishwa na Kipemba ambacho kina konsonanti 28.

Imeshaelezwa na wataalamu mbalimbali kuwa sauti za lugha ni majumui katika lugha zote ulimwenguni. Hata hivyo, kila lugha ina upekee wake kwa kuchota baadhi ya sauti hizo kulingana na utaratibu wa lugha hiyo. Kwa mfano, irabu za msingi ni 8 ambazo zinapatikana katika lugha mbalimbali ulimwenguni. Lakini, sio kila lugha inatumia irabu zote hizo 8. Inadaiwa kwamba ingawa lugha nyingi za binadamu huwa zina angalau irabu 5, lakini kuna baadhi ambazo zina irabu zaidi ya 5 na kuna nyingine zina irabu 3 tu (Massamba, 2012). Ukweli juu ya jambo hili haukuishia katika irabu pekee bali unajitokeza hata katika konsonanti. Kwani katika makala haya imebainika kuwa, Kipemba kina konsonanti 28 ambazo baadhi zinapatikana katika Kingazija na nyingine zinapatikana katika Kipemba pekee. Kadhalika Kingazija kimebainika kuwa na konsonanti 31 kati ya konsonanti hizo, ziko zinazopatikana katika Kipemba pia. Vilevile, kuna konsonanti ambazo zinapatikana katika Kingazija pekee.

Kiujumla, kati ya konsonanti 37 zinazoonekana katika orodha kuu kwenye Jedwali Na. 1, konsonanti 22 ambazo ni sawa na 60% zimejitokeza katika Kipemba na Kingazija. Aidha, konsonanti 15 pekee ndizo ambazo zimeonekana kusigana miongoni mwao. Kati ya hizo konsonanti 6 sawa na 16.2% zimejitokeza katika Kipemba pekee. Kwa upande mwingine sauti 9 sawa 24.3% zimejitokeza katika Kingazija pekee. Konsonanti mahususi zilizojitokeza katika Kipemba ni /č$^{h}$/, /t$^{h}$/, /p$^{h}$/, /ky/, /k$^{h}$/ na /ly/. Aidha, konsonanti pekee zilizobainika katika Kingazija ni /ts/, /dz/, /ʤ/, /β/, /θ/, /ð/, /ɣ/, /ʈ/ na /ɖ/. Aghlabu, tofauti ya sauti katika lugha/lahaja mbalimbali zinatokana na sababu za kifonolojia. Tumeshagusia hapo kabla kuwa kila lugha ina upekee wake, kwani huchota baadhi ya sauti kutoka katika kapu kuu la sauti za lugha zote ulimwenguni na huzisarifu kwa namna ya upekee kulingana na utaratibu wa lugha/lahaja husika.

**Ulinganishi wa Konsonanti /č/ na /ts/**

Maneno ya Kipemba na Kingazija yanatofautiana kimaumbo kwa matumizi ya konsonanti tofauti. Baadhi ya maneno ya Kipemba yanayotumia konsonanti /č/ katika Kingazija maneno hayohayo yanatumia konsonanti /ts/. Hebu tuangalie mifano ifuatayo katika Jedwali Na. 2:

**Jedwali Na. 2: Ulinganishi wa Konsonanti /č/ na /ts/ katika Kipemba na Kingazija**

| Na. | Kipemba | Kingazija | Kiswahi Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1. | di**ch**o | dzi**ts**o | jicho |
| 2. | ki**ch**wa | hi**ts**wa | kichwa |
| 3. | n**ch**i | mn**ts**i | nchi |
| 4. | n**ch**anga | m**ts**anga | mchanga |
| 5. | mabi**ch**i | mai**ts**i | mabichi |
| 6. | n**ch**ana | m**ts**ana | mchana |
| 7. | mbi**ch**i | mbi**ts**i | mbichi |
| 8. | **ch**eka | hu**ts**eha | cheka |
| 9. | ku**ch**wa | hu**ts**wa | kuchwa/tua |
| 10. | **ch**eza | hu**ts**apvuha | cheza |
| 11. | **ch**okoza | hum**ts**onga | chokoza |
| 12. | ma**ch**ozi | ma**ts**ozi | machozi |
| 13. | **ch**imba | hu**ts**imba | chimba |
| 14. | **ch**inja | **ts**indza/hu**ts**indza | chinja |
| 15. | **ch**echemea | **ts**heza/hu**ts**eheza | chechemea |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Jedwali Na. 2, limeonesha tofauti ya konsonanti za Kipemba na Kingazija ambazo zinarejeleana. Konsonanti hizo zimejitokeza hivyo kwa kutegemea utamkaji wake. Kimatamshi, /č/ ni kizuio-kwamizi hafifu cha kaakaa gumu na /ts/ ni kwamizi hafifu cha ufizi. Konsonati hizo zinakaribiana sana kutokana na sifa zake za jinsi ya kuzitamka na ukuruba wa mahali pa kuzitamka, kwani ufizi na kakaa gumu ni ala zinazokaribiana sana kiukaaji. Hebu tuchunguze mifano katika maneno yafuatayo:

| **Kipemba** | **Kingazija** |
|---|---|
| di***ch***o | dzi***ts***o |
| ki***ch***wa | hi***ts***wa |
| n***ch***i | mn***ts***i |
| n***ch***anga | m***ts***anga |
| ***ch***eka | hu***ts***eha |

Mabadiliko hayo, kama yalivyojitokeza katika maneno hapo juu, yanaonesha kuwa kila ilipojitokeza konsonanti /č/ katika Kipemba katika Kingazija imejitokeza [ts]. Hivyo basi, maneno haya ingawa yanaonekana kuwa ni tofauti kiumbo na

kimatamshi lakini kwa hakika, ni ya aina moja kwa sababu yote yanarejelea kitu kimoja na sauti zake pia zinarejeleana. Hii inatokana na ukweli kwamba katika taaluma ya fonolojia kama anavyodai Massamba, (2011) kuna michakato ya kiusilimisho ambayo sababu za kutokea kwake zinaweza kuelezeka kifonolojia. Kwani tunaweza kusema, mabadiliko fulani yametokea kutokana na sababu mahususi katika mazingira fulani ya kifonolojia. Mazingira ambayo yanaweza kusababisha kuathiriana kwa sauti ama zilizo jirani au zilizo mbali kidogo. Hata hivyo, kuna michakato mingine hutokea ambayo si ya kiusilimisho. Katika michakato hiyo hatuwezi kusema imetokana na kuathiriana kwa sauti fulani katika mazingira fulani. Mara nyingi mabadiliko kama hayo yanatokana na utaratibu wa lugha/lahaja mahususi kutokana na sababu mbalimbali kama vile athari za kimazingira yaliyowazunguka watumiaji wazawa wa lugha/lahaja husika kama yanavyojitokeza katika Kipemba na Kingazija.

## Ulinganishi wa Konsonanti /š/ na /ts/

Wakati mwingine konsonanti /š/ hutumika badala ya /č/ katika Kipemba ambayo pia hurejelea sauti /ts/ katika Kingazija. Tuchunguze mifano katika Jedwali Na. 3:

**Jedwali Na. 3: Ulinganishi wa Sauti /š/ na /ts/ katika Kipemba na Kingazija**

| Na. | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1 . | **sh**ana | hu**ts**ana | chana |
| 2. | n**sh**a | n**ts**a | ncha |
| 3. | **sh**ingo | n**ts**ingo | shingo |
| 4. | **sh**ongo | n**ts**ongo | chongo |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Kulingana na data iliyopo katika Jedwali Na. 3, tumebaini kuwa maneno yote ya Kipemba yanaonesha kuwa na konsonanti /š/ ambapo katika Kingazija konsonanti /ts/ imetumika badala ya /š/ Hii ni kudhihirisha kuwa konsonanti hizo zinakaribiana sana kimatamshi, pia, ziko jirani katika mahala pa kuzitamka. Kwa kuwa /š/ ni kikwamizi cha kaakaa gumu na /ts/ ni kwamizi cha ufizi, ni dhahiri kuwa kutakuwa na urahisi wa utamkaji wake. Tuangalie mifano ifuatayo:

| **Kipemba** | **Kingazija** |
|---|---|
| ***sh***ana | hu***ts***ana |
| ***sh***a | n***ts***a |
| ***sh***ingo | ***ts***ingo |
| ***sh***ongo | ***ts***ongo |

Katika mifano hiyo imebainika kuwa konsonati /š/ katika Kipemba inabadilika na kuwa /ts/ katika Kingazija. Kutokana na matumizi ya konsonanti /č/ na /š/ katika Kipemba kutofautiana na konsonanti /ts/ katika Kingazija kama yanavyonekana katika Jedwali Na. 2 na 3 hapo juu, tunabaini kuwa konsonanti /ts/ katika Kingazija ina konsonati mbili zinazorejeleana nazo katika Kipemba ambazo ni /č/ na /š/. Hata

hivyo, pamoja na tofauti hizo zinaonesha mfanano mkubwa kwa sababu konsonanti hizo ni mrejeo ambazo zimeunda maneno mnasaba.

**Ulinganishi wa Konsonanti /ɟ/ na /ʤ/**

Kipemba kina konsonanti /ɟ/ ambayo inajitokeza kama /ʤ/ katika Kingazija na hivyo kuyafanya maumbo hayo yaonekane kuwa ni tofauti. Hebu tuangalie mifano iliyomo katika Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na. 4: Ulinganishi wa Konsonanti /ɟ/ na /ʤ/ katika Kipemba na Kingazija**

| Na. | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1. | **j**ando | **dj**ando | jando |
| 2. | **j**oto | **dj**otro | joto |
| 3. | jua | hu**dj**uwa | jua/elewa |
| 4. | **j**ua | **dj**uwa | jua |
| 5. | ma**j**i | ma**dj**i | maji |
| 6. | **j**ana | **dj**ana | jana |
| 7. | **j**aa | hu**dj**aya | jaa |
| 8. | **j**ahazi | **dj**ahazi | jahazi |
| 9. | **j**imbi | **dj**imbi | jimbi |
| 10. | **j**ini | **dj**ini | jini |
| 11. | m**j**i | m**dj**i | mji |
| 12. | n**j**omba | m**dj**omba | mjomba |
| 13. | nfere**j**i | mfere**dj**i | bomba |
| 14. | nkongo**j**o | mkongo**dj**o | mkongojo |
| 16. | n**j**ugu | n**dj**ugu | njugu |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Mifano ya maumbo ya maneno yaliyoorodheshwa katika Jedwali Na. 4, inadhihirisha kuwa /ɟ/ katika Kipemba imetumika badala ya /ʤ/ katika Kingazija. Hivyo hizo zote ni konsonanti za aina moja ambavyo ni vizuio-kwamizi ghuna vya kakaa gumu. Tungalia mifano ifuatayo:

| **Kipemba** | **Kingazija** |
|---|---|
| ***j***oto | ***dj***otro |
| ***j***ua | ***dj***ua |
| ***j***ini | ***dj***ini |
| n***j***omba | m***dj***omba |

Data hiyo inaonesha kuwa konsonanti /ɟ/ katika maneno ya Kipemba imebadilika kuwa /ʤ/ katika Kingazija. Hii ina maana kwamba konsonti hizo zina uhusiano kwa sababu umbo la ndani ni sawa zinatofautiana katika umbo la nje tu. Huu ni ushahidi tosha kuwa Kipemba na Kingazija zina uhusiano wa karibu. Hivyo, sauti hizo zinarejeleana na hayo yote ni yanayotokana na lugha chanzi moja.

### Ulinganishi wa Konsonanti /g/ na /ʤ

Tunabaini vilevile kuwa konsonanti /g/ katika Kipemba inarejelea konsonanti /ʤ/ katika Kingazija. Tuchunguze mifano ifuatayo:

**Jedwali Na. 5: Ulinganishi wa Konsonati /g/ na /ʤ/ katika Kipemba na Kingazija**

| Na. | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1. | **g**unia | **dj**uniya | gunia |
| 2. | ntun**g**i | mtsun**dj**i | mtungi |
| 3. | n**g**ia | in**dj**ia | ingia |
| 4. | -in**g**i | -in**dj**i | -ingi |
| 5. | man**g**i | men**dj**i | mengi |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Katika mifano iliyopo katika Jedwali Na. 5 tunabaini kujitokeza kwa konsonanti /g/ katika Kipemba ambapo katika Kingazija imejitokeza kama /ʤ/. Hii ni kwa sababu kuwa konsonanti /g/ ni kipasuo ghuna cha kaakaa laini na /ʤ/ ni kizuio-kwamizi ghuna cha kakaa gumu. Hivyo, konsonanti hizo zinakaribiana kutokana na ukaribu wa mahali pa matamshi na jinsi ya kuzitamka. Tazama mifano ifuatayo:

| **Kipemba** | **Kingazija** |
|---|---|
| ***g***unia | ***dj***unia |
| in***g***ia | in***dj***ia |
| ntun***g***i | mtsu***dj***i |
| man***g***i | men***dj***i |

Katika data hiyo tunabaini konsonanti /g/ inayotumika katika Kipemba kutofautiana na konsonanti /ʤ/ katika Kingazija. Kwa mantiki hiyo, konsonanti /g/ ya Kipemba imetumika kama konsonanti mbadala /ʤ/ katika Kingazija. Aidha, konsonati /ʤ/ katika Kingazija inarejelewa na konsonati /ɟ/ na /g/ katika Kipemba kama zinavyoonekana katika Jedwali Na. 4 na 5. Hivyo, konsonati zote hizo zinarejeleana na kuyafanya maumbo hayo yawe sawa ingawa yanaonekana tofauti kiothografia.

### Ulinganishi wa Sauti [z] na [dz]

Katika Kipemba kuna ujirejeleaji wa konsonanti /z/ kwa /dz/ katika Kingazija. Baadhi ya maneno ya Kipemba ambayo yanachukua konsonanti /z/ katika Kingazija hutumia konsonanti /dz/ badala ya /z/. Mifano ifuatayo inaonesha jinsi konsonanti hizo zinavyorejeleana:

**Jedwali Na. 6: Ulinganishi wa Sauti [z] na [dz] katika Kipemba na Kingazija**

| Na. | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1. | **z**icho | **dz**itso | jicho |
| 2. | **z**ino | **dz**inyo | jino |
| 3. | mi**z**igo | mi**dz**o | mizigo |
| 4. | **z**iwa | **dz**iwa | ziwa la maji |
| 5. | pan**z**i | mban**dz**i | panzi |
| 6. | n**z**i | n**dz**i | nzi |
| 7. | An**z**uani | N**dz**uwani | Anzuani |
| 8. | kwen**z**i | kwen**dz**u | ndege |
| 9. | Mwivi/mwi**z**i | mwi**dz**i | mwizi |
| 10. | n**z**a**z**i | m**dz**a**dz**e | mzazi |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Data ya utafiti ambayo imeorodheshwa katika Jedwali Na. 6, inaonesha kuwa kikwamizi ghuna cha ufizi /z/ katika Kipemba kimekaliwa badala yake na kikwamizi ghuna cha ufizi /dz/ katika Kingazija. Tuchunguze mifano ifuatayo kutoka katika Jedwali hapo juu:

| **Kipemba** | **Kingazija** |
|---|---|
| *z*icho | ***dz***icho |
| *z*ino | ***dz***inyo |
| n*z*i | n***dz***i |
| n*z*a*z*i | n***dz***a***dz***e |

Konsonanti hizo zimeweza kubadilishana nafasi kutokana na urahisi wa kuzitamka kwa sababu zinakaribiana katika utamkaji wake. Pia, sauti hizo zote zinapatikana katika sehemu moja ambayo ni ufizi. Hivyo, mpishano wa konsonanti hizo ni jambo la kawaida kwa watumiaji wazawa wa lugha/lahaja wanaoishi katika mazingira tofauti ya kijiografia.

### Ulinganishi wa Konsonanti /ɟ/ na /dz/

Mara nyingine tunaona ukiukwaji wa konsonanti /ɟ/ katika Kipemba kubadilishana nafasi na /dz/ katika Kingazija. Baadhi ya maneno ya Kipemba yenye sauti /ɟ/ hujitokeza kama konsonanti /dz/ katika Kingazija. Tuangalie maumbo ya maneno yafuatayo ambayo konsonati hizo zimejitokeza katika Kipemba na Kingazija:

**Jedwali Na. 7: Ulinganishi wa Sauti /ɟ/ na /dz/ katika Kipemba na Kingazija**

| Na. | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1. | n**j**iwa | n**dz**iwa | njiwa |
| 2. | n**j**ano | **dz**in**dz**anu | njano |
| 3. | n**j**aa | n**dz**aya | njaa |
| 4. | n**j**iya | n**dz**iya | njia |
| 5. | n**j**o | n**dz**o | njoo |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Jedwali Na. 8 linaonesha kuwa maneno yaliyobainishwa katika Kipemba yana sauti /ɟ/ ambapo katika Kingazija imetumika konsonanti /dz/. Kujitokeza kwa konsonanti hizo katika Kipemba na Kingazija kunatokana na jinsi sauti hizo zinavyoweza kuwa rahisi kuzitumia na kuweza kurejeleana. Konsonati hizo, /ɟ/ na /dz/ ni za vizuio-kwamizi ghuna vya ufizi. Tuchunguze maneno yafuatayo:

| **Kipemba** | **Kingazija** |
|---|---|
| n***j***iwa | n***dz***iwa |
| n***j***aa | n***dz***aya |
| n***j***ia | n***dz***iya |
| n***j***o | n***dz***o |

Mabadiliko hayo ni ya kawaida kwa lugha/lahaja zenye chimbuko moja. Aghalabu mabadiliko hayo huwa yanasababishwa na mijongeo ya watu pamoja na mwachano na makutano yao kutokana na sababu za kutafuta maisha. Vilevile, katika Jedwali Na. 6 na 7 tunabaini konsonati /dz/ katika Kingazija inarejelewa na konsonati mbili katika Kipemba ambazo ni /z/ na /ɟ/. Kimsingi, tofauti zote za kimatamshi zinazojitokeza katika maneno hayo hazuii maelewano baina ya wazungumzaji wao. Sababu kubwa ya kusigana kwake kimatamshi ni kutokana na kujibainisha kwa kujitofautisha na wazungumzaji wa lugha/lahaja nyingine.

### Ulinganishi wa Konsonanti [k] na [h]

Kipemba kimedhihirisha ujitokezaji wa /k/ katika maumbo yake ambapo Kingazija konsonati hiyo hutamkwa /h/ badala ya /k/. Tufuatilie mifano iliyopo katika Jedwali Na. 8:

**Jedwali Na. 8: Ulinganishi wa Konsonanti /k/ na /h/ katika Kipemba na Kingazija**

| Na. | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1. | **k**ichwa | **h**itswa | kichwa |
| 2. | n**k**ono | m**h**ono | mkono |
| 3. | **k**inywa | **h**anywa | kinywa |
| 4. | pa**k**a | pa**h**a | paka |
| 5. | **k**ulya | **h**ula | kula |
| 6. | **k**unwa | **h**unwa | kunywa |
| 7. | **k**ufa | **h**ufa | kufa |
| 8 | nyo**k**a | nyo**h**a | nyoka |
| 9 | che**k**a | hutse**h**a | cheka |
| 10. | pi**k**a/injika | pi**h**a | pika |
| 11. | an**k**a | lam**h**a | amka |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Tukiichunguza vema data katika Jedwali Na. 8, tunabaini kuwa /k/ katika maumbo ya Kipemba haijioneshi katika Kingazija, badala yake hujitokeza konsonanti /h/. Hali hiyo imetokea kwa sababu konsonanti hizo hazipishani sana

kiutamkaji na pia mahali pa kuzitamkia. Mathalani, /k/ ni konsonanti ya kipasuo hafifu cha kakaa laini na /h/ ni kikwamizi ghuna cha koromeo. Hivyo kutokana na hali hiyo konsonanti hizo zinaweza kubadilishana nafasi kiurahisi katika matamshi. Tuangalie mifano ifuatayo kutoka katika Jedwali Na. 8.

| **Kipemba** | **Kingazija** |
|---|---|
| ***k***ichwa | ***h***itswa |
| n***k***ono | m***h***ono |
| pa***k***a | pa***h***a |
| ***k***ufa | ***h***ufa |

Kwa namna nyingine tunaweza kusema kuwa tofauti hizo za konsonanti zilizojitokeza zinaashiria mchakato wa ujulikanao kama ukwamizaji. Inawezekana kulitokea mabadiliko ya sauti ambapo sauti ya asili kutoka Mame-Bantu yawezekana kuwa ilikuwa /k/ ambayo ni kipasuo hafifu cha kakaa laini kikapitia mabadiliko ya kuwa /h/ kikwamizi cha koromeo katika mchakato wa ukwamizaji. Hivyo, hali hii inaonesha kwamba Kipemba na Kingazija zinatokana na asili ya mame-lugha moja.

### Ulinganishi wa Sauti /k/ na /š/

Wakati mwingine, kuna utokeaji wa konsonanti /k/ katika maumbo ya Kipemba ambapo katika Kingazija sauti hiyo haionekani. Maumbo ya Kingazija yanatumia konsonanti /š/ badala ya /k/. Hebu tuchunguze mifano katika Jedwali Na. 9:

**Jedwali Na. 9: Ulinganishi wa Sauti /k/ na /š/ katika Kipemba na Kingazija**

| Na. | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1. | ntun**k**e | mwanam**sh**e | mwanamke |
| 2. | n**k**iya | m**sh**iya | mkia |
| 3. | shi**k**iyo | shi**sh**iyo | sikio |
| 4. | **k**ibuno | **sh**iwuno | kiuno |
| 5. | si**k**ia | yi**sh**iya | sikia |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Kutokana na mifano iliyomo katika Jedwali Na. 9, tunagundua kuwa konsonanti /k/ ambayo ni kizuio hafifu cha kakaa laini katika maneno ya Kipemba hujibainisha kama konsonanti /š/ katika Kingazija. Mifano ifuatayo inadhihirisha hali hiyo:

| **Kipemba** | **Kingazija** |
|---|---|
| ntun***k***e | mwanam***sh***e |
| n***k***ia | m***sh***iya |
| ***k***ibuno | ***sh***iwuno |
| si***k***ia | yi***sh***iya |

Mabadiliko hayo ya konsonanti /k/ ya kizuio hafifu cha kaakaa laini katika Kipemba yamesababisha konsonati hiyo ibadilike na kuwa /š/ katika Kingazija. Konsonati ya asili ya Mame-Bantu pengine ilikuwa /k/, konsonati ya kipasuo hafifu

cha kakaa laini katika Kipemba. ambayo ilibadilika na kuwa /š/ kiwamizo cha ufizi katika Kingazija kutokana na mchakato wa ukwamizaji.

### Ulinganishi wa Konsonanti /d/, /t/ na /ɖ/

Konsonanti /d/ na /t/ katika Kipemba inajitokeza kama /ɖ/ katika Kingazija. Kadhalika, yako baadhi ya maneno ya Kipemba ambayo wakati mwingine badala ya /d/, hutumika konsonanti /t/ ambayo pia hubadilishana na Kingazija kwa konsonanti hiyohiyo /ɖ/. Utokeaji wa konsonanti hizo unaonekana katika mifano ifuatayo:

**Jedwali Na. 10: Ulinganishi wa Konsonanti /d/, /t/ na /ɖ/ katika Kipemba na Kingazija**

| Na. | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1. | pun**d**a | pun**dr**a | punda |
| 2. | n**d**izi | n**dr**ovu | ndizi |
| 3. | n**d**uwaro | n**dri**waro | nduaro |
| 5. | n**t**umuume | m**dr**umme | mwanamme |
| 6. | n**t**u | m**dr**u | mtu |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Katika mifano hiyo iliyomo katika Jedwali Na. 10, tunaweza kugundua kuwa konsonanti /d/ ambayo ni kipasuo ghuna cha ufizi katika baadhi ya maumbo ya Kipemba hujitokeza /ɖ/ ya Kingazija ambacho ni kimadende cha ufizi. Aidha, konsonanti /t/ ya kipasuo hafifu cha ufizi katika Kipemba hubadilika na kuwa /ɖ/. Hebu fuatilia mifano hii:

| **Kipemba** | **Kingazija** |
|---|---|
| pun***d***a | pun***dr***a |
| n***d***izi | n***dr***ovu |
| n***t***umuume | m***dr***umme |
| n***t***u | m***dr***u |

Katika mabadiliko hayo, tunabaini konsonati mbili za Kipemba /d/ na /t/ ambazo zinabadilika na kuwa /ɖ/ katika Kingazija. Konsonanti /d/ ya kipasuo ghuna cha ufizi imebadilka na kuwa kimadende cha ufizi /ɖ/. Kadhalika, konsonanti /t/ ya kipasuo hafifu cha ufizi imebadilika kuwa kimadende /ɖ/ cha ufizi. Mabadiliko ya konsonanti hizo yamejitokeza katika mazingira ya kutanguliwa na nazali ya ufizi /n/ katika Kipemba na nazali ya midomo /m/ katika Kingazija.

### Ulinganishi wa Konsonanti /k/ na /r/

Kuna mazingira ambayo maneno mengine ya Kipemba hutumia konsonanti /k/ badala ya /r/ inayotumiwa katika Kingazija. Hebu tuchunguze mifano ifuatayo katika Jedwali Na. 11:

**Jedwali Na. 11: Ulinganishi wa Konsonanti /k/ na /r/ katika Kipemba na Kingazija**

| Na. | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1. | ku**t**i | ku**r**i | kuti |
| 2. | m**t**o | m**r**o | mto |
| 3. | nyo**t**a | nyo**r**a | nyota |
| 4. | mafu**t**a | mafu**r**a | mafuta |
| 5. | m**t**i | m**r**i | mti |
| 6. | ma**t**e | ma**r**e | mate |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Kutokana na data katika Jedwali Na. 11, tunaona kuwa konsonanti /k/, kipasuo hafifu cha kaakaa laini katika Kipemba kimebadilika na kuwa konsonanti ya kimadende /r/ katika Kingazija. Tuangalie mifano ifuatayo:

| **Kipemba** | **Kingazija** |
|---|---|
| ku***t***i | ku***r***i |
| nyo***t***a | nyo***r***a |
| m***t***o | m***r***o |
| m***t***i | m***r***i |

Mifano ya maumbo hayo yanadhihirisha pia mchakato wa ughunishaji kati irabu. Katika baadhi ya lugha mbalimbali ulimwenguni na lugha nyingi za Kibantu, baadhi ya konsonanti hasa za vipasuo zinapokuwa katikati ya irabu mbili hubadilika na kuwa ghuna iwapo hapo awali hazikuwa ghuna. Tukichunguza mifano ya maneno iliyopo hapo juu, tunabaini kuwa konsonati /k/ ambayo ni kipasuo hafifu cha kakaa laini katika Kipemba, imebadilika kuwa konsonanti ya /r/ ghuna ya kimadende katika Kingazija. Inawezekana Kingazija kimepata mabadiliko ya konsonanti hiyo kupitia mchakato huo. Kama tulivyotangulia kusema kuwa konsonanti zote hizo zimejitokeza katika mazingira maalumu ambayo ni.katikati baina ya irabu na irabu. Hata hivyo kuna vighairi ambapo konsonanti hiyo imejitokeza baina ya nazali na irabu kama ilivyo katika maneno 'mti' na 'mto' katika Kipemba na 'mri' na 'mro' katika Kingazija. Hata hivyo, konsonanti hizo zinarejeleana kwa kuwa zinaeleza dhana moja na zote zimetokea katika mazingira ya aina moja.

## Ulinganishi wa Sauti /t/ na /ţ/

Kuna utokeaji wa konsonanti /d/ katika Kipemba lakini konsonanti hiyo hubadilika na kuwa /ţ/ katika Kingazija. Hebu tuangalie mifano ifuatayo:

**Jedwali Na. 12: Ulinganishi wa Konsonanti /t/ na /ʈ/ katika Kipemba na Kingazija**

| Na. | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1. | **t**unda | **tr**undra | tunda |
| 2. | **t**ango | **tr**ango | tango |
| 3. | **t**andu | **tr**ambu | tandu |
| 4. | ko**t**i | ko**tr**i | koti |
| 5. | **t**embeya/enenda | hu**tr**embeya | tembe |
| 6. | **t**umbo | **tr**umbo | tumbo |
| 7. | **t**afuna | hu**tr**afunya | tafuna |
| 8. | n**t**ama | **tr**ama | mtama |
| 9. | ki**t**unguu | i**tr**unguu | kitunguu |
| 10. | sha**t**i | sha**tr**i | shati |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Jedwali Na. 12 linaonesha kuwa konsonanti /t/ ya kizuio hafifu cha ufizi katika Kipemba kimeirejelea konsonanti ya kimadende cha ufizi /ʈ/ katika Kingazija. Hebu tuchunguze maneno yafuatayo:

| **Kipemba** | **Kingazija** |
|---|---|
| ***t***unda | ***tr***undra |
| ***t***ango | ***tr***ango |
| n***t***ama | ***tr***ama |
| sha***t***i | sha***tr***i |

Katika data hiyo mabadiliko ya konsonanti /t/ na /ʈ/ katika Kipemba na Kingazija vilevile, yanatokana na mchakato wa ughunishaji. Kwani katika orodha ya maneno kwenye Jedwali Na. 12, kila ilipotumika konsonanti hafifu /t/ katika Kipemba, inakuwa sauti ghuna /ʈ/ katika Kingazija. Konsonanti hizo zote zimebadilika katika mazingira mbalimbali. Kwanza, mazingira ya kufuatiwa na irabu. Pili, konsonanti hizo zimejitokeza baina ya irabu na irabu kama inavyoonekana katika mifano hiyo. Hivyo, konsonanti hizo zinatambulika kuwa ni sauti mrejeo ambazo zimetumika katika maneno mnasaba ya Kipemba na Kingazija.

## Usilimisho wa Konsonati na Uchopekaji wa Viyeyusho

Maumbo ya Kipemba hudondosha nazali ambapo katika Kingazija nazali hiyo huchopekwa. Mara nyingine kiyeyusho kinadondoshwa katika Kipemba ambapo katika Kingazija kinachopekwa au kinyume chake. Hebu tutalii mifano katika Jedwali Na. 13:

**Jedwali Na. 13: Ulimisho wa Konsonanti na Uchopekaji wa Viyeyusho katika Kipemba na Kingazija**

| Na. | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1. | pua | **m**bua | pua |
| 2. | kamba | **n**kamba | kamba |
| 3. | pweza | **m**bweza | pweza |
| 4. | sungura | sungur**w**a | sungura |
| 5. | tausi | t**w**ausi | tausi |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Katika mifano ya Jedwali Na. 13, tunabaini kuwa kuna matumizi ya nazali ya midomo /m/ na ufizi na /n/ katika maneno ya Kingazija wakati ambapo katika Kipemba nazali hizo hazionekani. Tuangalie baadhi ya mifano iliyobainishwa katika Jedwali hapo juu:

| **Kipemba** | **Kingazija** |
|---|---|
| ***θ***pua | ***m***bua |
| ***θ***kamba | ***n***kamba |
| ***θ***pweza | ***m***bweza |
| sungura | sungur***w***a |
| tausi | t***w***ausi |

Data hiyo inadhihirisha nazali /m/ na /n/ katika maneno ya Kingazija. Katika Kipemba maneno yake hayabainiki kuwa na nazali hizo na badala yake yanaonekana kuwa umbo kapa '**θ**'. Aidha, baada ya kuingizwa nazali hizo katika Kingazija, konsonanti /p/ ambayo ni kipaso hafifu cha midomo imeimarishwa kuwa /b/ kipasuo ghuna cha midomo. Uimarishwaji huo umetokana na konsonati hafifu /p/ kubadilishwa kuwa konsonati ghuna /b/. Tofauti hizo za konsonati zimesababishwa na mchakato wa usilimisho unaohusu konsonanti ambayo ni nazali kutamkiwa mahali pamoja na konsonanti inayoifuatia. Mabadiliko hayo yanajidhihirisha katika data hiyo kwa sababu nazali /m/ ya midomo katika Kingazija imesababisha kufuatiwa na konsonanti ya midomo /b/ kama zilivyojitokeza katika maneno 'mbua' na 'mbweza'. Aidha, /n/ haikusababisha konsonanti /k/ kubadilika kwa kuwa zote zinatamkiwa kwenye ufizi kama katika neno 'nkamba'. Hivyo, mabadilko hayo yanadhihirisha kuwa nazali ikifuatiwa na konsonanti nyingine ya midomo inakuwa /m/, ikifuatiwa na konsonanti nyingine ya ufizi inakuwa /n/.

Maneno hayo ya Kipemba na Kingazija yanahusishwa na ngeli ya 10 ambayo viambishi vyake vya umoja na wingi huwa havibadiliki. Mara nyingi kiambishi 'n-' ndicho ambacho kinatumika katika umoja na wakati huohuo hutumika katika wingi. Baadhi ya wataalamu wanadai kuwa huenda kundi hili lilikuwa na kiambishi ngeli 'n-' lakini ama kilipotea au kudondoshwa kihistoria na kuachwa shina pekee katika nomino zisizoanza na kiambishi hiki kama ilivyo katika maneno ya Kipemba.

Vilevile, katika data hiyo, tunabaini mbadiliko ya maumbo ya Kingazija yaliyosababishwa na uchopekwaji wa kiyeyusho /w/. Kiyeyusho hicho kimechopekwa baina konsonanti /r/ na irabu /a/ pamoja na konsonanti /t/ na irabu /a/; 'sungurwa' na 'twausi' ambapo katika Kipemba uchopezi huo hauonekani katika maneno 'sungura' na 'tausi'.

### Ulinganishi wa Konsonanti zenye Mpumuo

Konsonanti 28 za Kipemba zilizobainishwa katika Jedwali Na.1 zimejumuishwa pamoja na zile ambazo zinachukua mpumuo kwa sababu mpumuo ni sifa bainifu ya baadhi ya lahaja mbalimbali za Kiswahili. Hivyo, ingawa mpumuo haujidhihirishi kama sifa bainifu ya sauti katika Kiswahili Sanifu, lakini katika Kipemba hujidhihirisha kama sifa mojawapo ya konsonanti. Konsonanti za mpumuo katika Kipemba hutumiwa zaidi na wazungumzaji wazawa ili kutofautisha maana anuwai za maneno. Tuchunguze Jedwali Na. 14 amabalo linaonesha tofauti ya maana katika konsonanti zenye mpumuo na ambazo hazina mpumuo katika Kipemba na ufafanuzi wake katika Kiswahili Sanifu:

**Jedwali Na. 14: Ulinganishi wa Konsonati zenye Mpumuo katika Kipemba na Kingazija**

| Otografia | Matamshi | Maana kwa Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|
| $p^h$ | $p^haa$ | aina ya mnyama wa porini |
| P | paa | kitendo cha kutoa samaki maganda |
| $t^h$ | $kat^ha$ | kitendo cha kutenganisha vitu sehemu mbili |
| T | kata | kifuu au kikopo kilichotiwa mpini ili kuchotea maji |
| $k^h$ | $k^hamba$ | samaki mdogo wa baharini mwenye miguu mingi na gamba laini |
| K | kamba | uzi uliotengenezwa kwa urefu unaotumika kwa kazi mbalimbali |
| $\check{c}^h$ | $ch^hanga$ | isio komaa |
| C | changa | vumbivumbi la udongo |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Tukichunguza Jedwali Na. 14, tunagundua kuwa matumizi ya mpumuo yanaleta athari kubwa katika Kipemba. Hii inatokana na sababu kuwa maneno yenye konsonanti za mpumuo yanatofautisha maana na yale ambayo hayana mpumuo. Hivyo, matumizi ya mpumuo yanachukuliwa kama sifa bainifu ya konsonanti katika Kipemba. Kwa upande wa Kingazija konsonanti zenye mpumuo hazikubainika. Hata hivyo, konsonanti [$\check{c}^{h,}$ $k^{h,}$ $p^h$ na $t^h$] za Kipemba zinabadilishananafasi na konsonanti [č, k, p na k] katika Kingazija kwa sababu zinafanana katika sifa za kimatamshi na mahali pa kuzitamka.

## Konsonanti zenye Athari ya Kigeni

Konsonanti 37 za Kipemba na Kingazija zilizobainishwa katika Jwedwali Na. 1 imebainika kuwapo kwa konsonanti zenye athari za kigeni. Konsonanti hizo mara nyingine zinatumika katika baadhi ya lahaja za Kiswahili, lugha za Kibantu pamoja na Kiswahili Sanifu. Konsonanti hizo ni: [θ, ð, ɣ na x] ambazo zinatokana na maneno ya mkopo yenye athari ya lugha ya Kiarabu. Hata hivyo, katika Kipemba, konsonanti hizo huwa hazijitokezi hata kwenye maneno hayo ya mkopo wakati katika Kingazija zinatumika kama zilivyo katika lugha ngeni. Tuchunguze mifano katika Jedwali Na. 15:

**Jedwali Na. 15: Konsonanti zenye Athari ya Kigeni katika Kipemba na Kingazija**

| Matamshi | Otografia | Kipemba | Kingazija | Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|---|
| [θ] | | samanini | thamanini | themanini |
| [ð] | h | zambi | dhambi | dhambi |
| [x] | kh | wahera | akhera | akhera |
| [ɣ] | gh | hafla | ghafla | ghafla |

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2020)

Katika mifano iliyojitokeza kwenye Jedwali Na. 15, inaonesha kuwa konsonanti zenye athari ya Kiarabu zinabadilishwa kimatamshi katika Kipemba. Maneno kama 'thamanini', 'dhambi', 'akhera' na 'ghafla' hutamkwa 'samanini', 'zambi', 'wahera' na 'hafla'. Katika Kingazija, sauti hizo za kigeni zinatamkwa kama zilivyo katika lugha ya Kiarabu. Hata hivyo, pamoja na kuwa katika Kipemba konsonanti hizo zinabadilika kimatamshi, bado kuna uhusiano. Kwa mfano, sauti [θ, ð, ɣ na x] zote ni vikwamizi vya meno na kakaa laini na sauti [s, z, h] nazo pia ni vikwamizi vya meno na koromeo. Bila shaka, tumeweza kubaini kuwa sauti hizo zinakaribiana sana katika sifa zake za kimatamshi na mahala pa kuzitamkia. Kwa maana hiyo, kurejeleana katika lugha ni jambo la kawaida. Hivyo, hiyo sio sababu ya kukifanya Kipemba na Kingazija zionekane kuwa ni lugha mbili tofauti ambazo hazina asili moja.

## Hitimisho

Kifonolojia kuna mshabaha mkubwa wa konsonanti baina ya Kipemba na Kingazija. Hii inadhihirisha kuwa jamii za wazugumzaji hao kuna wakati ziliwahi kukutana ndiyo maana kukawa na uhusiano kutokana na mfanano wake wa sauti kama ambavyo tumezibainisha. Katika Nadharia ya Isimu Historia-Linganishi sauti hizo zinajulikana kama sauti mrejeo. Hata hivyo, tofauti ndogondogo zilizojitokeza zimechombezwa na umbali wa kimasafa uliopo baina ya Kisiwa cha Pemba na Kisiwa cha Ngazija na hivyo, kuzifanya lugha zao ziathiriwe na mazingira yaliyowazunguka. Aidha, tofauti hizo zinaonesha kuwa jamii za Wapemba na Wangazija baadaye zilitengana kutokana na sababu mbalimbali za kibinadamu kama vile, kutafuta maisha, biashara n.k. Hivyo, tunathubutu kusema kwamba

Kipemba na Kngazija zina uhusiano wa kimnasaba kwa sababu zinatokana na mame-lugha moja.

**Marejeleo**


Chiraghdin, S. na M. Mnyampala. (1977). *Historia ya Kiswahili.* Nairobi: Oxford University Press.

Chomsky, N. na M. Halle. (1968). *Sound Pattern of English*. New York: Harper and Row.

Jakobson, R. na M. Halle. (1951). *Preliminaries to Speech Analysis*. Massachusetts: MIT Press.

Jones, W. (1786). "A Dissertation on the Orthography of Asiatick Words in Roman Letters". *Katika Asiatick Researches.* 1:1-56.

Juma, H. K. (2019). "Ulinganishi wa Kihistoria na Kiisimu wa Lahaja za Kiamu, Kimvita, Kipemba, Kitumbatu na Kimicheweni." Tasnifu ya Uzamivu. (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kipacha, A. (2003). *Lahaja za Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.* Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2007). *Kiswahili Origins and the Bantu Divergence-Convergence Theory.* Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2011). *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2012). *Misingi ya Fonolojia*. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2017). *Historia ya Kiswahili: Mtazamo Mpya 100KK hadi 2000BK*. Dar es Salaam: Kiswahili Development Limited.

Nurse, D. na T. J. Hinnebusch. (1993). *Swahili and Sabaki.* California: California University.

Nurse, D. na T. Spear. (1985). *The Kiswahili: Reconstructing the History and Language of an African Society.* Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Nurse, D. (1989). *Is Comorian Swahili?Being an Examination of the Diachronic Relationship between Comorian and Coastal Swahili.* Paris: Editions Recherche sur les Civilisations.

Swadesh, M. (1952). "Lexicostatistic Dating of Prechistoric Ethnic Contacts". Katika *Preceeding American PhilosophicalSociety*,96: 452-463.